



Lakini Herode  
hangeweza kumdhuru  
Mwana wa Mungu!  
Alionywa katika ndoto,  
Yusufu alichukua  
Mariamu na Yesu kwa  
usalama huko Misri.

19



Wakati Herode  
alipokufa Yusufu  
alileta Mariamu na  
Yesu kutoka  
Misri.

Waliishi katika mji mdogo wa  
Nazareti, karibu na bahari ya Galilaya.


20

Kuzaliwa kwa Yesu

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Biblia,  
hupatikana katika  
Mathayo 1-2, Luka 1-2

"Malango ya maneno yako yatoa nuru."  
Zaburi 119:130

21



22



Zambi kanyingika ngwenyi thunlingi yuma ipi,  
yokakwamba ngwenyi shili, nyi fweto yashili kufwa.

Zambi kathuzanga cikuma, kathumine mwanenyi, yusu,  
kufwa hakulusu hanga apwe khuka yamilonga yethu  
yashili, yesu ejile nyimwono wenyi nyikuhilukamo kwilu.  
Kashika zambi mathukonekena shili jyethu.

Ngwe unafuphu ngwe ulikonekene shilijye, hanjika kuli  
zambi ye ngwee, zambi tata ngwafulyela ngwami yesu  
kangufwilile, haphwala kali mutolo, tweya mumbunge  
yami hanga ungukonekene shili jyami, hanga ngupwe nyi  
mwono, hanga ngukathwame nyiyena myaka yeswe,  
ngukwase hanga ngupwe mwanee. Amen. Yowano 3:16

Tanga mbimbiliya nyikuhanjika nyizambi  
tangwa hitangwa.

23

Chokwe


Zambi kanyingika ngwenyi thunlingi yuma ipi,  
yokakwamba ngwenyi shili, nyi fweto yashili kufwa.

Zambi kathuzanga cikuma, kathumine mwanenyi, yusu,  
kufwa hakulusu hanga apwe khuka yamilonga yethu  
yashili, yesu ejile nyimwono wenyi nyikuhilukamo kwilu.  
Kashika zambi mathukonekena shili jyethu.

Ngwe unafuphu ngwe ulikonekene shilijye, hanjika kuli  
zambi ye ngwee, zambi tata ngwafulyela ngwami yesu  
kangufwilile, haphwala kali mutolo, tweya mumbunge  
yami hanga ungukonekene shili jyami, hanga ngupwe nyi  
mwono, hanga ngukathwame nyiyena myaka yeswe,  
ngukwase hanga ngupwe mwanee. Amen. Yowano 3:16

Tanga mbimbiliya nyikuhanjika nyizambi  
tangwa hitangwa.

24



25

Imeandikwa na: Edward Hughes  
Imeonyeshwa na: M. Maillot; Alastair Paterson

Ilitafsiriwa na: www.christian-translation.com  
Imebadilishwa na: E. Frischbutter; Sarah S.

Hadithi ya 36 kati ya 60

**M1914.org**

**Bible for Children, PO Box 3, Winnipeg MB R3C 2G1 Canada**

Leseni: Una haki ya kunakili au kuchapisha hadithi hii, mradi hauuzi.



1

2

"Hii inawezaje kuwa?" msichana yule alishangaa akaluliza. "Sijawahi kuwa na mwanaume yeyote." Malaika alimwambia Mariamu mtoto atatoka kwa Mungu. Hakutakuwa na baba wa kibinadamu.



3

Malaika kisha akamwambia Mariamu kwamba binamu yake Elizabeth alikuwa akizaa mtoto katika uzee wake. Huu pia ulikuwa muujiza. Mara tu baadaye, Mariamu alimtembelea Elizabeth. Walimsifu



4

Mungu pamoja.

Mariamu alikuwa ameolewa na mwanamume aliyetwa Yusufu. Yusufu alihuzunika alipojua Mariamu alikuwa anatarajia mtoto. Alidhani mtu mwingine ni baba.



5

Katika ndoto, malaika wa Mungu alimwambia Yusufu kwamba mtoto huyu alikuwa Mwana wa Mungu. Yusufu alikuwa amsaidie Mariamu kumtunza Yesu.



6

Yusufu alimwamini na kumtii Mungu. Alitii pia sheria za nchi yake. Kwa sababu ya sheria mpya, yeye na Mariamu waliondoka kwenda mji wao, Bethlehemu, kulipa ushuru.



7

Mariamu alikuwa tayari kupata mtoto wake. Lakini Yusufu hakuweza kupata chumba mahali popote. Nyumba zote za wageni zilikuwa zimejaa.



8

Mwishowe Yusufu alipata zizi. Hapo, Mtoto Yesu alizaliwa. Mama yake alimlaza kwenye hori la ng'ombe, mahali ambapo chakula cha wanyama kilikuwa kikiwekwa kawaida.



9

Karibu, wachungaji walinda mifugo yao iliyokuwa ikilala. Malaika wa Mungu alitokea na kuwaambia habari hizo za ajabu. "Umezaliwa leo katika mji wa Daudi Mwokozi Ambaye ni



Kristo Bwana. Utakuta Mtoto amelazwa horini."

10

Ghafla, malaika wengi zaidi mkali walitokea, wakimsifu Mungu na kusema, "Utukufu kwa Mungu aliyee juu na duniani amani,



mapenzi mema kwa wanadamu."

11

Wachungaji walienda haraka kwenye zizi. Baada ya kumwona Mtoto huyo waliwambia kila mtu walikutana na kile malaika walisema juu ya Yesu.



12

Siku 40 baadaye, Yusufu na Mariamu walimleta Yesu kwenye hekalu huko Yerusalemu.



Hapo mtu mmoja aliyetwa Simeoni alimsifu Mungu kwa Mtoto, wakati mzee Anna, mtumishi mwingine wa Bwana, alishukuru.

13

Wote wawili walijua kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu, Mwokozi aliyeahidiwa. Yusufu alitoa dhabihu kwa ndege wawili. Hii ndio iliyokuwa sadaka ya sheria ya Mungu ilisema watu masikini wanapaswa kuleta wakati wanapomletea Bwana mtoto mchanga.



14

Wakati mwingine baadaye, nyota maalum iliwaongoza Wenye hekima kutoka nchi ya



Mashariki kwenda Yerusalemu. "Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi?" waliuliza. "Tunataka kumwabudu."

15

Mfalme Herode alisikia kuhusu Wajanja. Akiwa na shida, aliwauliza wamwambie wanapompata Yesu. "Ninataka kumwabudu Yeye pia," Herode alisema. Lakini alikuwa akisema uwongo. Herode alitaka kumwua Yesu.



16

Nyota iliwaongoza Wenye Hekima kwa nyumba ile halisi ambayo Maria na Yusufu waliishi na Mtoto mchanga. Wakipiga magoti kwenye ibada, wasafiri hao walimpa Yesu zawadi nyingi za dhahabu na marashi.



17

Mungu aliwaonya Wenye Hekima warudi nyumbani kwa siri. Herode alikasirika sana. Aliamua kumuamgiza Yesu, mtawala yule mwovu aliua watoto wote wa kiume huko Bethlehemu.



18